



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.AC.209/366/02 "C"/25

Tarehe: 27.10. 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale alipokea kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/521/01"B"/73 ya tarehe 16 Septemba, 2021 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa nafasi (04) za Watendaji wa Vijiji III.

Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI (04)

Ngazi ya Mshahara ni TGS B1 sawa na Shilingi 390,000/= kwa mwezi

SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti NTA LEVEL 5 katika moja ya fani zifuatazo; - Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya sanaa katika chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo – Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Mtendaji na mshauri wa Halmashauri ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya Maendeleo ya kijamii na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

- ii. Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
- iii. Mlinzi wa amani na msimamizi wa wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iv. Kutafsiri sera, Utaratibu na kusimamia utekelezaji wa sharia ndogondogo za Halmashauri katika Kijiji.
- v. Kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika Kijiji chake na kuziwasilisha kwenye Kata.
- vi. Kuongoza vikao vya maendeleo ya Kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- vii. Kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji.
- viii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo wa Kitaalamu katika Kijiji.

MASHARTI YA MWOMBAJI

- i. Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45 awe tayarikufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.
- ii. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma.
- iii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne (IV) au sita (VI), cheti cha kuzaliwa na Picha 2 (passport size) za hivi karibuni pamoja na CV Ikionesha Sanduku la posta na namba za simu
- iv. Mwombaji anatakiwa aambatanishe vyeti vilivyo sainiwa na kupigwa mhuri (CERTIFIED COPY) wa Mwanasheria au Mahakama.
- v. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 12/11/2021 saa 9:30 alasiri aidha maombi yote yawasilishwe kwa Anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 352
NYANG'HWALE

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri www.nyanghwaledc.go.tz
na katika mbao za matangazo.



Rajabu B. Mmunda
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

NYANG'HWALE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P. 352
NYANG'HWALE,

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Geita,
Barua pepe: ded@nyanghwaledc.go.tz Tovuti: www.nyanghwaledc.go.tz